

## Huduma zinazopatikana kabla ya kipindi cha makato yako kufikiwa

Bima zote zinalipia matibabu ya kinga kabla kipindi cha makato yako hakijafikiwa.



**Bima za Cascade Care**  
zinalipia huduma zaidi kabla ya kipindi cha makato yako kufikiwa.

Huduma hizi zinajumuisha:



Matibabu ya kinga



Matibabu ya msingi, kumwona daktari kwa ajili ya ugonjwa au jeraha



Huduma za afya ya akili



Kuandikiwa dawa za kawaida



Matibabu ya haraka, ukihitaji matibabu ya haraka mara moja lakini huna dharura kama shambulio la moyo.

## Najisajili kwa njia gani?

### Piga



1-855-923-4633  
TTY/TDD: 1-855-627-9604  
Saa: 7:30 AM hadi 5:30 PM  
Msaada unapatikana kwa lugha zaidi ya 200.

### Wasiliana



Weka miadi na chanzo cha kuaminika katika jumuiya yako.



Tafuta navigator au broker wa kukusaidia mtandaoni kupitia [wahealthplanfinder.org](http://wahealthplanfinder.org). Bofya kitufe cha Get Support.

### Tembelea



Tambaza msimbo wa QR Tembelea tovuti kupitia: [wahealthplanfinder.org](http://wahealthplanfinder.org)

## Bima ya Afya Inapatikana kwa Kila Mtu!

Kila mtu anayeishi katika jimbo la Washington anaweza kununua bima ya afya na meno kupitia *Washington Healthplanfinder*.



**Watu wenyewe hali zote za uhamiaji wanakaribishwa!  
Hii ni programu ya wote, bila kujali mambo ya vibali.**

### Usalama wako ni muhimu kwetu:

- Kupata bima ya afya hakuathiri hali yako ya uhamiaji au maombi ya uraia kwa ajili yako, familia yako, au yeyote anayeishi pamoja nawe.
- Taarifa zako binafsi hazitatumwa kwa madhumuni ya ushurutishaji wa uhamiaji.
- Taarifa kuhusu hali yako ya uhamiaji zinatumika tu kubaini aina gani za bima za afya una ustahiki wa kuzinunua.

## Bima ya afya ni nini?



Bima ya afya ni makubaliano ambayo unaingia pamoja na kampuni ya bima. Kampuni ya bima inakubali kulipia baadhi au garama zako zote za kila mwezi badala ya malipo yako ya kila mwezi.

## Kwa nini niwe na bima ya afya?

Bima ya afya inasaidia kulipia huduma ya afya iwe unaitumia bima kuhakikisha unadumu mwenye afya njema au unaitumia unapoumwa.

## Inagharimu kiasi gani?

Gherama ya kununua bima ya afya inategemea na vitu kama kipato chako, ukubwa wa familia, na mahali unapoishi. Unaweza kufuzu bima ya **Cascade Care Savings**, jambo linalomaanisha jimbo litalipa sehemu ya bima yako ya afya. Ukipuzu, kiasi unacholipia matibabu ya afya kitapungua.

## Bima ya afya inafanyaje kazi?

Unalipa ada ya kila mwezi ikiwa unahitaji huduma ya afya. Kisha ukihitaji huduma za afya, utatozwa huduma hizi kwa bei ya punguzo.

## Vigezo vya Bima ya Afya

### Ada ya Bima

Kila mwanachama analipa ada ya kila mwezi inayoitwa "premium". Bei ya "premium" yako inategemea na aina ya bima yako ya afya.



### Makato

Bima yako ya afya inaanza kukusaidia kulipia bili zako baada ya "kufikia kiasi chako cha makato". Bima zote zinalipia huduma fulani, kama ukaguzi wa kiafya, kabla kipindi cha makato hakijafikiwa.

### Malipo shirikishi na Bima shirikishi

Hizi ni gherama unazolipa ukienda kwa daktari. Malipo yako shirikishi ni kiasi kisichobadilika (\$1-\$50). Bima yako shirikishi ni asilimia ya gherama ya huduma. Aina yako ya bima ya afya inalipia ziara yote ya kumwona daktari.

### Mifano ya Bili za Matibabu

Unaumwa na unahitaji matibabu. Bili yako ya matibabu ni \$10,000.

Huna bima.

*Jumla unayolipa kutoka mfukoni (out-of-pocket): \$10,000*

Ukiwa na bima unalipa kidogo zaidi.

Bima inalipa: \$7,960

*Jumla unayolipa (kutoka mfukoni): \$2,040*

- Makato: \$2,000
- Malipo shirikishi: \$40

## Aina gani za bima za afya zinapatikana?

Kuna ngazi tatu za bima za afya zinazopatikana kuitia Washington Healthplanfinder: Shaba, Fedha, na Dhahabu. Kiasi kinacholipwa na kampuni yako ya bima ya afya inategemea na ngazi gani unachagua. Ngazi ya Shaba inalipa takribani 60%, ngazi ya Fedha inalipa takribani 70%, na ngazi ya Dhahabu inalipa takribani 80% ya bili zako za matibabu.

### Shaba

Bima hizi zinagharimu kidogo zaidi kwa mwezi lakini zinalipia gherama kidogo unapohitaji matibabu.

### Fedha

Bima hizi zinakinga zaidi ya gherama zako ukihitaji matibabu lakini zinaweza kugharimu zaidi. Ukipuzu Cascade Care Savings bima hizi zinaweza kugharimu kidogo zaidi kuliko bima za Shaba.

### Dhahabu

Bima hizi zinagharimu zaidi kwa mwezi lakini zinalipia gherama zaidi ukihitaji matibabu. Ukipuzu Cascade Care Savings na una mahitaji makubwa ya huduma ya afya bima hizi zinaweza kukufaa zaidi.

## Angalia nembo ya Cascade Care!



Bima za Cascade Care zinatoa thamani zaidi kwa gherama ndogo. Yaani, malipo yako ya ada ya bima yanakupa faida zaidi!